CHUO KIKUU CHA SOKOINE CHA KILIMO

# MATUKIO YA SUA

## Kuanzia Julai hadi Septemba, 2022



www.sua.ac.tz @sokoineuniversityofagriculture

"Ardhi ni Hazina"

# Mhe. Jaji Warioba akaribisha Baraza jipya na kupongeza Baraza lililopita



*Mkuu wa Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo Mhe. Jaji Joseph Sinde Warioba akiongea wakati wa hafla ya uzinduzi wa Baraza jipya la Chuo.*

Mkuu wa Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo Mhe. Jaji Joseph Sinde Warioba amepongeza baraza la Chuo kwa tathlitha ya kumi na mbili na kukaribisha Baraza jipya la Chuo kwa Tathlitha ya kumi na tatu.

Mhe. Warioba alitoa pongezi hizo wakati wa hafla ya uzinduzi wa baraza jipya ambapo aliwashukuru wajumbe wa Baraza la Tathlitha ya kumi na mbili na kuwakaribisha wajumbe wapya siku ya Ijumaa Agosti 19, 2022 katika Ukumbi wa Taasisi ya Elimu ya Kujiendeleza ICE, SUA.

Akizungumzia kuhusu utendaji kazi wa Tathlitha ya 12 ambayo imehudumu kwa muda wa miaka mitatu tangu mwaka 2019 ambapo ndipo ugonjwa wa UVIKO -19 uliingia nchini, Mkuu huyo wa Chuo alisema analipongeza Bazara hilo kwa kazi kubwa waliyoifanya kwa kuongoza na kusaidia kuendesha vizuri masomo kwa wanafunzi wa Chuo hicho.

Jaji Warioba alisema japo kuna changamoto nyingi Baraza jipya linapaswa kusaidia katika kubana matumizi ya fedha zilizopo kwa kujifunza kutumia kile kidogo kilichopo kwa ufanisi mkubwa ili kusonga mbele na kufikia malengo ya Chuo.

Awali akizungumza mbele ya Mkuu wa Chuo, Makamu Mkuu wa Chuo cha Sokoine cha Kilimo SUA Prof. Raphael Chibunda naye hakusita kutoa pongezi kwa Baraza la Tathlitha ya 12 kwa kazi kubwa waliyoifanya katika kipindi hicho cha miaka 3 tangu Julai 1, 2019 hadi June 30, 2022.

Prof. Chibunda alitaja baadhi ya mafanikio yaliyopatikana katika Baraza la Tathlitha ya 12 ikiwa ni pamoja na mikutano ya kuidhinishwa kwa muundo mpya wa Chuo pamoja na upanuzi wa shughuli za Chuo kama kuongeza Kampasi ya mkoani Katavi (Kampasi ya Mizengo Pinda), Tunduru Pamoja na Shamba la mfano la Kampasi ya Edward Moringe, na pia Chuo kimetoa watafiti bora nchini ambapo mara mbili mfululizo Chuo kimetoa Mtafiti namba moja ambaye ni Prof. Ludovic Kazwala.

Naye Katibu wa Baraza Bi. Lunyamadzo Gillah aliongoza zoezi la utoaji vyeti kwa wajumbe wa Baraza lililopita. Pia aliongoza zoezi la kukabidhi vitendea kazi kwa wajumbe wa Baraza jipya.

Hafla hiyo ilihudhuriwa na watu mbalimbali akiwemo Mkuu wa Chuo cha SUA, Makamu Wakuu wa Chuo, Wajumbe wa Baraza la Tathlitha ya 12 na 13, Wakuu wa Ndaki mbalimbali, Wakuu wa Idara na Vitengo mbalimbali.



**“Ardhi ni Hazina”**

# SUA na Wizara ya Afya kushirikiana na Wadau wa Tiba Asili



*Mkurugenzi wa Shahada ya Uzamili, Utafiti na Uhawilishaji wa Teknolojia kutoka Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo SUA Prof. Esron Karimuribo akiongea wakati wa Kongamano la kwanza la Kisayansi la Tiba Asili Tanzania.*

Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo kwa kushirikiana na Wizara ya Afya kimeahidi kufanya kazi bega kwa bega na wadau mbalimbali waliopo katika mnyororo wa Thamani wa bidhaa za Tiba Asili kwaajili ya kuibua Bunifu na kupata suluhisho la Kisayansi kuhusu changamoto zilizopo kwenye mnyororo wa thamani wa biashara ya bidhaa za Mimea Dawa nchini.

Hayo yalibainishwa siku ya Jumatatu Agosti 29, 2022 na Mkurugenzi wa Uzamili, Utafiti na Uhawilishaji wa Teknolojia kutoka Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo SUA Prof. Esron Karimuribo wakati akimuwakilisha Naibu Makamu Mkuu wa Chuo upande wa Taaluma na Tafiti ambaye alikuwa mgeni rasmi kwenye Kongamano la Kwanza la Kisayansi la Tiba Asili Tanzania la siku mbili linalofanyika SUA Kampasi ya Edward Moringe (Kampasi Kuu).

Alisema uwepo wa Kongamano hilo la Kisayansi kuhusu Tiba Asili ya Mwafrika lililowakutanisha Wadau mbalimbali waliopo katika mnyororo wa Thamani wa bidhaa za Tiba Asili wakiwemo Wakulima wazalishaji, Wavunaji, Watengenezaji, Wauzaji wa jumla na rejareja, Taasisi zinazosimamia Ubora, Watunga Sera na Watafiti upo kwenye moja ya majukumu na malengo ya uanzishwaji wa SUA.

Prof. Karimuribo alisema wanaamini lengo la Kongamano hilo ni kuibua Bunifu na kupata suluhisho la Kisayansi kuhusu changamoto zilizopo kwenye mnyororo wa thamani wa biashara ya Bidhaa ya za Mimea Dawa nchini ili iwe endelevu na iweze kutoa mchango mkubwa kwenye kipato cha Wananchi kwa ujumla.

"Tunathamini sana mchango wa Sekta hii na tunaamini tukishirikiana kwa pamoja tutafika mbali hivyo nasisitiza katika swala la Ubunifu ili kuweza kuwa na dawa Asili katika mfumo ambao unaweza kuupeleka kwenye "Pharmacy" ili tuweze kujua kilichopo ndani, dozi ni kiasi gani hata hivyo watafiti wameamua kujiongeza na kufanya dawa hizi za Asili kuwa katika muundo kama wa dawa nyingine tunazotumia" alisema Prof Karimuribo.

Aidha Prof. Karimuribo aliwahakikishia wadau wa Kongamano hilo la kwanza la Kisayansi la Tiba Asili Tanzania kuwa SUA kwa kushirikiana na Serikali ya Tanzania itakuwa nao bega kwa bega katika kuhakikisha kuwa yatokanayo na Kongamanola hilo yanapewa kipaumbele katika kazi zao za Utafiti, Mafunzo na kuwa endelevu ili kuboresha Bidhaa hizo za Tiba Asili.

Kwa upande wake Dkt Paul. Mhame kutoka Wizara ya Afya alikiomba Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo SUA kuwasaidia kufanya Utafiti wa namna ya kulima na kupanda Miti Dawa katika kiwango kinachokubalika.




**"Ardhi ni Hazina"**

**Baadhi ya picha katika Kongamano la Kwanza la Kisayansi la Tiba Asili Tanzania la siku mbili linalofanyika SUA Kampasi ya Edward Moringe (Kampasi Kuu).**

















**"Ardhi ni Hazina"**

# Wanafunzi wa SUA wapata mafunzo Hifadhi ya Taifa ya Tarangire



*Wanafunzi wa Shahada ya Kwanza wa Kozi ya Uhifadhi Wanyama Pori wa Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo wakipata mafunzo kwa vitendo katika Hifadhi ya Taifa ya Tarangire iliyopo mkoani Manyara.*

Chuo Kikuu Cha Sokoine cha Kilimo kimetoa mafunzo kwa vitendo kwa Wanafunzi wa Shahada ya Kwanza wa Kozi ya Uhifadhi Wanyama Pori katika hifadhi ya Taifa ya Tarangire iliyopo mkoani Manyara siku ya Jumanne tarehe 7 June, 2022 na kumalizika tarehe 05 Julai 2022.

Akizungumzia mafunzo hayo, Dkt. Richard Samson Joachim kutoka Idara ya Upasuaji na Uzalishaji Wanyama iliyopo Ndaki ya Tiba ya Mifugo na Sayansi Shirikishi SUA alisema nia kubwa ya mafunzo hayo ni kuwajengea uwezo Wanafunzi kuwa karibu na Wanyamapori pamoja na kuhakikisha usalama wao pamoja na Wanyama unakuwepo kwa kuwapa mbinu sahihi za kuwakamata Wanyama hao.

"Nia kubwa ya mafunzo haya kwa vitendo ni kuwajengea uwezo wa kuwa karibu na Wanyamapori kujifunza jinsi gani unaweza kutunza Wanyama Pori lakini vilevile kuhakikisha kwamba usalama wako wewe na usalama wa mnyama unakuwepo, hivyo tulikuwa na shughuli nyingi kama kukamata Wanyama tulifanikiwa kuwakamata Wanyama kadhaa kama Pundamilia, Nyumbu, Simba na Tembo", alisema Dkt. Joachim

Naye Afisa Muhifadhi kutoka hifadhi hiyo ya Tarangire Kitengo cha Tiba ya Wanyama Bw. Godwin Olomi alisema kuwa wamewapokea wanafunzi hao na kuwapa maelezo kuhusiana na tahadhari katika maeneo ya kukamatia Wanyama na nini cha kufanya baaada ya mnyama kukamatwa akiwa chini.

"Wanafunzi tumewapokea na tumewapa maelekezo vizuri na wamefuata maelekezo na wamepata kitu kwa sababu tunategemea wao ndio wahifadhi na wengine watakuja kusimamia hata vitengo hivi, kwa hiyo wanatakiwa wafahamu hata vitendo vinavyofanyika ili kusudi huko mbeleni na wao waje kufanya haya mambo", alisema Bw. Olomi.

Mafunzo hayo yalihusisha kukamata Wanyama kwa kutumia vifaa mbalimbali, kutibu Wanyama ambao wamepata matatizo, namna ya kutofautisha Wanyama kwa jinsi zao pamoja na kujua namna uoto wa hifadhi unavyotunzwa ili kuwafanya Wanyama wawe salama.



# Uzinduzi wa Kigoda cha Oliver R. Tambo, SUA




*Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknlojia Mhe. Omary Kipanga akiongea wakati wa uzinduzi wa Kigoda cha Oliver Tambo katika Ukumbi wa Baraza la Chuo, SUA. Kampasi ya Edward Moringe.*

Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo kimeshiriki katika uzinduzi wa Kigoda cha Oliver Tambo cha Afrika kinachohusiana na tafiti za magonjwa ya kuambukizwa yatokanayo na virusi. Uzinduzi huo umefanyika siku ya Jumatatu tarehe 15 Agosti, 2022 katika Ukumbi wa Baraza la Chuo, SUA.

Akizungumza mara baada ya kufungua rasmi Kigoda hicho Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknlojia Mhe. Omary Kipanga ambaye ndiye alikuwa Mgeni rasmi akimuwakilisha Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia alisema kuwa lengo kuu la tafiti hizo ni kuhakikisha kuwa zinakwenda kutumika Serikalini, kupitia Taasisi yake ya Sayansi na Teknolojia COSTECH ambayo inaratibu tafiti hizo kwa kuzitoa kwenye makaratasi na kuzipeleka kwenye matumizi.

“katika kigoda hiki tumeweza kupata fedha zaidi ya Bilioni 2 ambazo zitatusaidia katika kufanya tafiti mbalimbali hasa zile zinazojikita katika kuibua changamoto tulizokuwa nazo hasa za magonjwa yatokanayo na virusi yanayoathiri Binadamu pamoja na Wanyama”, alisema Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo, Sayansi na Teknolojia

Mara baada ya uzinduzi huo, Mwenyekiti wa Kigoda hicho
Prof. Gerald Misinzo kutoka Taasisi ya SACIDS, SUA alisema kuwa Kigoda hicho kina mkakati unaolenga kuikwamua nchi yetu kutoka katika magonjwa yanayoathiri ufugaji au mifugo pamoja na afya ya binadamu ili kuharakisha utekelezaji wa maono ya Tanzania ya kimaendeleo na Bara la Afrika kufikia 2060 pamoja na utekelezaji wa maendeleo ya Dunia ya kumkwamua kila mwananchi kuwa katika Maisha bora kufikia 2030.

“Malengo yetu makubwa ni kupambana na maadui watatu wa kitaifa ambao ni ujinga, maradhi na umaskini lakini hasa ni kupigana na maradhi yanayosababishwa na magonjwa ya kuambukizwa ili kuboresha afya ya binadamu pamoja na mifugo. Hivyo tunatumia teknolojia ya kisasa kuyabaini magonjwa hayo ili kuweza kupata suluhu na kuyaondoa pamoja na kukomboa watu na mifugo kutokana na magonjwa hayo”, alisema Prof. Misinzo.

Vilevile alipendekeza jinsi ya kukabiliana na magonjwa hayo kwa haraka na kwa gharama nafuu ambapo ni pamoja na matumizi ya Afya moja, ikiwa na maana kuwa sekta ya mifugo ishirikiane na sekta ya binadamu katika utendaji wake wa kazi.

Namna nyingine ni kuweza kubaini magonjwa hayo kulekule kwenye jamii kwa kutumia njia za kidijitali mfano simu janja zinazoweza kutumika kuwasilisha taarifa za magonjwa na mwisho ni kufika sehemu husika na vitendea kazi vya kisasa ambavyo vinachakata vinasaba na kuweza kubaini ni mdudu gani anasababisha ugonjwa katika eneo husika.

Kigoda cha Olive R. Tambo ni miongoni mwa Vigoda 10 barani Afrika na kimoja kati ya viwili vilivyopo nchini Tanzania. Vigoda hivyo vimeanzishwa kwa madhumuni ya kumpa heshima Oliver R. Tambo aliyekuwa mwenyekiti wa Chama cha Ukombozi wa Afrika Kusini katika kutimiza miaka 100 tangu kuzaliwa kwake.

**Baadhi ya picha katika tukio la uzinduzi wa Kigoda cha Oliver Tambo uliofanyika Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo Kampasi ya Edward Moringe**













**"Ardhi ni Hazina"**

# SUA kuchangia CHAHITA ili kuboresha Elimu ya Hisabati




***Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo Prof. Raphael Chibunda akiongea katika Warsha ya 56 ya Kitaifa ya Hisabati Tanzania na Mkutano Mkuu wa Chama uliofanyika Kampasi ya Solomon Mahlangu SUA.***

Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo kimeahidi kutoa kiasi cha sh. 1,000,000/= kila Mwaka kwa ajili ya kukiunga mkono Chama cha Hisabati Tanzania (CHAHITA) katika harakati wanazozifanya kwa ajili ya kuboresha Elimu ya Hisabati nchini ikiwemo utoaji wa Mafunzo kwa Walimu wa Hisabati.

Hayo yalibainishwa na Makamu Mkuu wa Chuo hicho Prof. Raphael Chibunda wakati akimwakilisha Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia Prof. Adolf Mkenda ambaye alikuwa Mgeni Rasmi katika ufunguzi wa Warsha ya 56 ya Kitaifa ya Hisabati Tanzania na Mkutano Mkuu wa Chama uliofanyika Kampasi ya Solomon Mahlangu SUA.

Alisema CHAHITA kinahitaji angalau Sekta ya Umma ili kukipa nguvu katika kushawishi Walimu wa Somo la Hisabati kuhudhuria Warsha mbalimbali zinazotoa mafunzo katika kuboresha mbinu za ufundishaji na ujifunzaji hivyo atashirikiana bega kwa bega na Uongozi wa Chama hicho ili kuona wanachoweza kufanya katika kuishawishi Wizara ya Elimu lakini kuishawishi (TAMISEMI) katika kusaidia chama hicho kwenye shughuli zake.

Prof. Chibunda alisema Uongozi wa Chama unafanya kazi kubwa sana katika kutatua hali mbaya ya ufaulu kwenye somo la Hisabati lakini bado kuna kazi kubwa ya kufanya ikiwemo kujenga uelewa kwa jamii kuhusiana na somo hilo.

“Wanahesabu hawa ni wa muhimu sana lakini ujuzi wa hesabu walionao hauwapi wadau kama walivyo Wahandisi na Wakandarasi kuwashawishi kwamba hii kampuni bila Hesabu isingesimama inaweza kutuchukua muda kwa hiyo tutahitaji ***Intervation*** ya angalau Sekta ya kiserikali kuweza kusaidia hasa pande za pembezoni ambapo kuna shida kubwa katika somo hili la hesabu hivyo tunahitaji nguvu ili walimu wa Hesabu kutoka maeneo yote ya Tanzania kuhudhuria Warsha kama hizi” alisema Prof. Chibunda.

Kwa upande wake Mwenyekiti wa Chama cha Hisabati Tanzania (MAT/CHAHITA) Bi. Betinasia Manyama alisema changamoto wanazokumbana nazo ni pamoja na ufaulu hafifu wa somo la hisabati hasa kwa ngazi ya Msingi na Sekondari ambapo kunachangiwa hasa na upungufu wa walimu kwa ngazi zote za Elimu ambapo wameelemewa na idadi kubwa ya vipindi.

Changamoto nyingine ni ukosefu wa Fedha za kuendeshea kazi mbalimbali ndani ya chama ikiwemo nauli kwaajili ya kuwapatia waalimu kwenda kufundishia mwezi wa tatu kila mwaka pamoja na Walimu wa Hisabati kukosa Hamasa kutokana na kazi nyingi huku Mshahara ukiwa ni uleule kwa walimu wote bila kujali mwalimu wa somo hili ana vipindi vingi na somo lake linahitaji ufuatiliaji wa hali ya juu.

“Wastani wa waliofaulu katika miaka tisa iliyopita katika mtihani wa Hisabati wa kitaifa kwa Shule za msingi ni asilimia 31.86 na katika Shule za Sekondari ni asilimia 76.46, kwa mfano ufaulu wa Hisabati kwa kidato cha nne mwaka 2021 ni 19.54% hivyo ni vyema Serikali kulipa somo la Hisabati umuhimu maalum maana ndio nguzo ya masomo yote hasa masomo ya Sayansi na pia bila Hisabati hakuna Wahandisi na hivyo hakuna Viwanda”, alisema Bi. Betinasia Manyama.

**“Ardhi ni Hazina”**

**Baadhi ya picha katika ufunguzi wa Warsha ya 56 ya Kitaifa ya Hisabati Tanzania na Mkutano Mkuu wa Chama uliofanyika Kampasi ya Solomon Mahlangu SUA**





# Vijana waongezewa ujuzi na fursa zinazohusu uchumi wa kidijitali, SUA




*Dkt. Neema Sumari kutoka Idara ya Teknolojia ya Habari, SUA akieleza juu ya maswala ya ujasiriamali na namna yanavyoweza kuongeza kipato cha vijana na kuimarika kiuchumi.*

Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo kimeshiriki katika kuandaa jukwaa la kuwezesha kizazi kijacho na mabingwa wa kidijitali kwa kuwaangazia fursa za kuongeza ujuzi wao wa kidijitali na pia fursa za kazi na kuongeza mapato katika uchumi wa kidijitali.

Jukwaa hilo lilifunguliwa na Mkurugenzi wa Kurugenzi ya Uzamili, Utafiti, Uhaulishaji wa Teknolojia na Ushauri wa Kitaalamu Prof. Esron Karimribo siku ya Alhamisi Agosti 18, 2022 katika ukumbi wa MLT9 Kampasi ya Edward Moringe, SUA.

Prof. Karimribo alisema kuwa tukio la leo ni la muhimu sana, ambapo jukwaa hilo ni muhimu katika kuwajengea uwezo vijana kwa upande wa jiditali. Jukwaa hilo litaenda kujadili maswala ya ajira na ujasiriamali kwa vijana ili kuwasaidia kuleta mabadiliko katika uchumi wa kidijitali na pia litawasaidia vijana kujua namna bora ya kutengeneza fursa pamoja na ujasiriamali ili kujiongezea kipato

“kama tunavyojua dunia inaenda kwa kasi, hivyo tunaweza kuchagua kwenda na kasi hiyo kwa kubuni teknolojia mpya zitakazotusaidia. Sisi SUA tumefanikiwa kuwa na mifumo ya teknolojia mbalimbali ambayo imefanyiwa Utafiti na Wataalamu wetu na hivyo kusaidia katika kuleta maendeleo ya uchumi wa kidijitali”, alisema Prof. Karimuribo.

Naye Dkt. Alcardo Alex Barakabitze kutoka Idara ya Teknolojia ya Habari SUA, alisema kwamba majukwaa kama haya yanasaidia kutoa ujuzi kwa vijana pamoja na kutoa mchango mkubwa katika kuongeza uchumi wa kidijitali. Lakini pia amewashauri vijana kujiunga katika majukwaa kama haya ili kuweza kupata fursa zinazopatika huko.

Kwa upande wake Dkt. Neema Sumari kutoka Idara ya Teknolojia ya Habari, SUA alieleza juu ya maswala ya ujasiriamali na namna yanavyoweza kuongeza kipato cha vijana na kuimarika kiuchumi.

“kuwa mjasiriliamali ni tofauti na kuwa mfanyabiashara kwakuwa mjasiriamali anajitoa kufanya kitu chochote kile ili kuondokana na umaskini. Hivyo unapokuwa na wazo la kufanya ili kujiongezea kipato unapaswa kujua mambo muhimu yatakayo husika katika wazo lako hilo ilikuweza kufikia malengo yako”, alisema Dkt. Sumari

Jukwaa hili la vijana lililoandaliwa na SUA kwa kushirikiana na wadau wengine ni moja kati ya majukwaa ya kuhamasisha maendeleo kwa vijana ili kujikwamua kiuchumi, likiwa na kauli mbiu isemayo mabadiliko ya nafasi za kidijitali kwa vijana.




*Dkt. Alcardo Alex Barakabitze kutoka Idara ya Teknolojia ya Habari SUA, akichangia mada katika jukwaa la kuwezesha kizazi kijacho na mabingwa wa kidijitali*

# Baadhi ya picha katika Jukwaa la kuwezesha kizazi kijacho na mabingwa wa kidijitali lililofanyika Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo Kampasi ya Edward Moringe





# Prof. Chibunda awapongeza wanawake SUA



*Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo Prof. Raphael Chibunda akiwasalimia Wafanyakazi waliojitokeza katika Semina iliyoandaliwa na Chama cha Wafanyakazi Washirika na Wanataaluma Watafiti (RAAWU).*

Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo Prof. Raphael Chibunda amewapongeza wafanyakazi na wanafunzi wa jinsi ya kike na kuwashukuru kwa mchango wao katika maendeleo ya Chuo.

Pongezi hizo alizitoa katika semina iliyoandaliwa na Chama cha Wafanyakazi Washirika na Wanataaluma Watafiti (RAAWU) tawi la SUA siku ya Alhamisi tarehe 30/06/2022 katika ukumbi wa Multipurpose SUA.

Pia alitumia nafasi hiyo kuwaasa wanafunzi wa kike kujitahidi kuondokana na mazingira hatarishi katika masomo yao pamoja na kutumia muda wao vizuri pindi wawapo chuoni.

“Idadi ya wanafunzi wakike chuoni ni ndogo ukilinganisha na idadi ya wanafunzi wa kiume, lakini wanafunzi wa kike wameonekana kufanya vizuri licha ya idadi yao kuwa ndogo hii inatokana na nidhamu waliyonayo wanafunzi wa kike katika kufuata taratibu na kanuni zilizowekwa na Chuo.” alisema Prof. Chibunda.

Mada mbalimbali zinazomuhusu mwanamke ziliwasilishwa kutoka kwa watoa mada ambapo wanawake walikumbushwa juu ya thamani yao wakiwa kazini na chuoni ili kuleta maendeleo. Waliongeza kuwa thamani ya mwanamke inaonekana katika kile anachokifanya au kukiwakilisha katika eneo lake la kazi. Lakini pia walikumbushwa kuhusu ajira na sheria ya kazi, ambapo wanawake wanapaswa kutambua haki zao pindi wawapo kazini na chuoni.

Naye Mwenyekiti wa RAAWU Bi. Enesa Mlay alisema kuwa wanawake wanapofanya kazi wanapaswa watambue haki zao, pia wanapaswa watambue wajibu wao kwaajili ya kuleta ufanisi na maendeleo katika Chuo.

Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo kina asilimia 42 ya wanafunzi wa kike kati ya wanafunzi wote waliopo chuoni na wahadhiri wa jinsi ya kike wasiopungua 98 kati ya wahadhiri wasiopungua 502. Wanafunzi wa kike wameonekana kufanya vizuri kwa miaka miwili mfululizo, ambapo mwaka jana zilitolewa zawadi 222 kwa wanafunzi waliofanya vizuri kwenye masomo yao ambapo 72% ilikuwa jinsi ya kike.



*Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo Prof. Raphael Chibunda (katikati waliokaa) akiwa katika picha ya pamoja na wafanyakazi waliojitokeza katika Semina iliyoandaliwa na Chama cha Wafanyakazi Washirika na Wanataaluma Watafiti (RAAWU) .*

# Maonesho ya Ubunifu wa mavazi SUA



***Baadhi ya washiriki  wakionesha mavazi ya Kitamaduni katika maonesho ya mavazi yaliyofanyika katika ukumbi wa Multipurpose uliopo Kampasi ya Edward Moringe (Kampasi Kuu).***

Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo kupitia Idara yake ya Lishe ya Binadamu na Sayansi za Walaji ambapo wanafunzi wa Shahada ya Sayansi ya Familia na Ulaji wa Idara hiyo wameweza kuandaa maonesho ya mavazi yaliyofanyika katika ukumbi wa Multipurpose uliopo Kampasi ya Edward Moringe siku ya Ijumaa tarehe 24 Juni 2022.

Maonesho hayo ambayo yalikuwa ni moja ya mtihani kwa vitendo kwa wanafunzi wanaosoma Shahada ya Sayansi ya Familia na Ulaji yaliyoambatana na Ubunifu wa aina mbalimbali wa mavazi kwa kutumia bidhaa ambazo zimekwisha tumika na zile zinazopatikana kwa urahisi katika mazingira ya Chuo kwa mfano makaratasi, mifuko ya kubebea bidhaa (mifuko ya Magufuli), mifuniko ya chupa za maji, magunia, manyoya ya kuku na ngozi za wanyama.

“Shahada hii kimsingi inamuandaa mwanafunzi kutumia mazingira yaliyopo na vifaa ambavyo vinapatikana na kuweza kuviandaa katika njia ambayo inaweza kumletea faida”. Alisema Rasi wa Ndaki ya Kilimo, Prof.  Benard Chove.

Pia ubunifu huo uliwakilisha mavazi kutoka katika baadhi ya kabila za kitanzania kama kabila la Wagogo, Wamasai, Wahaya na Wazaramo ziliwakilishwa kwa mavazi yao ya asili. Mavazi hayo yalionesha kwa jinsi gani makabila hayo yanavyotumia mavazi yao ya asili katika matukio mbalimbali.

“watu wanalalamika sana hamna ajira, lakini vijana wanaweza kujiajiri hata ukiwa na mtaji mdogo na ukabuni vitu mbalimbali ambavyo vinaweza kukuingizia kipato”, alisema Furaha Mayanja mmoja wa washiriki mwanafunzi wa mwaka wa tatu.

Wabunifu wengi wanapata changamoto katika kutafuta malighafi za kutengenezea aina mbalimbali za mavazi pamoja na bidhaa nyingine.

Ubunifu uliooneshwa na wanafunzi kutoka Chuo cha Sokoine cha Kilimo umeweza kutanua wigo wa malighafi za bidhaa zinazotuzunguka na zile zilizokwisha muda wake kuweza kutumika katika kazi mbalimbali za kibunifu.



## Baadhi ya picha katika maonesho ya mavazi yaliyoandaliwa na Idara ya Lishe ya Binadamu na Sayansi za Walaji













# Prof. Chibunda: "Uwepo wa Maonesho ya TCU ni faida kwa Vyuo na Wanafunzi"



*Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo Prof. Raphael Chibunda akitoa neno la kushukuru kwa Tume ya Vyuo Vikuu nchini (TCU) wakati wa hafla ya kufunga rasmi maonesho ya sita ya Vyuo Vikuu Tanzania.*

Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA), Prof. Raphael Chibunda ameipongeza Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania (TCU) kwa kuandaa Maonesho ya Taasisi ya Elimu ya juu kwani Maonesho hayo yanaongeza wigo wa Taasisi hizo kuweza kujitangaza na pia ni fursa kwa Wanafunzi kukutana moja kwa moja na Vyuo Vikuu na kufanya Udahili.

Prof. Chibunda aliyasema hayo siku ya Jumamosi tarehe 23 Julai, 2022 katika Viwanja vya Mnazi Mmoja jijini Dar es Salaam wakati alipokuwa akitoa neno la kushukuru katika hafla ya kufunga rasmi Maonesho hayo ya siku sita.

Aidha amehimiza uwepo wa maonesho hayo kila mwaka huku akiipongeza Wizara ya Elimu kupitia Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania (TCU) kwa kuwezesha kufanyika kwa Maonesho hayo kwa mafaniko makubwa.

Awali mapema katika ziara yake ya kutembelea mabanda ya washiriki Katibu Mkuu Wizara ya Elimu Dkt Francis Michael alikipongeza Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA) kwa kuanziasha Programu mbalimbali za ujasiriamali zinazowawezesha wanafunzi wa Chuo hicho kujihusisha katika kazi za uzalishaji Mali na kujikwamua kiuchumi.

Akiwa katika Banda Hilo Dkt. Michael alijionea kazi mbalimbali zinazofanywa na wajasiriamali hao ikiwemo bidhaa za ushonaji pamoja na kilimo.

Maonesho ya Taasisi za Elimu ya Juu, Sayansi na Teknolojia yalifunguliwa rasmi Julai 18, mwaka huu na Waziri Mkuu Mhe. Kassim Majaliwa Majaliwa na kufikia tamati yake Julai 23,2022.



*Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Majaliwa K. Majaliwa (katikati) akiwa katika picha ya pamoja na baadhi ya Viongozi wa Taasisi ya Elimu ya juu nchini na Viongozi wengine wa Serikali wakati wa kufunga rasmi Maonesho ya Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania (TCU), 2022 katika viwanja vya Mnazi Mmoja jijini Dar es Salaam.*

**"Ardhi ni Hazina"**

# Baadhi ya picha za matukio mbalimbali kwenye Banda la SUA katika maonesho ya Vyuo Vikuu Tanzania (TCU), 2022













**“Ardhi ni Hazina”**

# SUA yazindua rasmi siku ya Bioteknolojia



*Mkurugenzi wa Shahada ya Uzamili, Utafiti, Uhaulishaji wa Teknolojia na Ushauri wa Kitaalam Prof. Esron Karimuribo akiongea na wadau waliojitokeza katika uzinduzi wa siku ya Bioteknolojia.*

Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo kupitia Taasisi yake ya Sayansi za Wanyama na Afya ya Jamii imezindua siku ya Bioteknolojia ambayo imetajwa kuwa siku muhimu katika tasnia ya Bioteknolojia.

Uzinduzi huo ulifanywa na Mkurugenzi wa Shahada ya Uzamili, Utafiti, Uhaulishaji wa Teknolijia na Ushauri wa Kitaalam Prof. Esron Karimuribo akimuwakilisha Mgeni rasmi ambaye ni Makamu Mkuu wa Chuo hicho siku ya Jumamosi tarehe 30 Julai, 2022 katika ukumbi wa Multipurpose Kampasi ya Edward Moringe (Kampasi Kuu).

Akiongea na Ofisi ya Mawasiliano na Masoko siku hiyo, Prof. Karimuribo alisema Bioteknolojia ni tasnia ambayo inaibukia kwa sasa na ni muhimu sana katika maendeleo ya Taifa kwasababu, kwa kutumia Teknolojia hiyo imekuwa msaada mkubwa katika kuhakikisha dawa mbalimbali kwaajili ya matibabu zinazalishwa na vilevile umuhimu wake unatambulika katika kutengeneza vitenganishi ambavyo vinatumika kwenye kutambua magonjwa ya aina mbalimbali.

"Lakini pia inapokuja kwenye uzalishaji tunafahamu kuwa tunahitaji vyakula vya kutosha kwa kutumia Teknolojia hii ya Bioteknolojia unaweza kuzalisha vyakula vingi kwa mpigo kwasababu unaweza ukaongeza tija ya vyakula na ubora wa vyakula lakini pia upande wa Mazingira inatusaidia sana wakati wa kuangalia mambo ambayo yanaendana na usafi wa Mazingira yetu". Alisema Prof. Karimurubo

Naye Mkuu wa Idara ya Biolojia, Parasitolojia pamoja na Bioteknolojia wa SUA Prof. Christopher Kasanga alisema wanabioteknolojia wamekutana na kuifanya siku hiyo kuwa maalum ili kujadiliana jinsi ya maendeleo ya Bioteknolojia yanavyoweza kusaidia katika kuleta maendeleo ya nchi na dunia kwa ujumla.

"tumejumuika na wanafunzi wa kozi hii ya Bioteknolojia ili waweze kutambua uhalisia wa Taaluma yao katika maendeleo ya Sayansi ya dunia kwa kuwa ndio Wanasayansi wa leo na kesho. Pia tumeona mambo ya msingi katika kutunza afya ya jamii kama vile kugundua visababishi vya magonjwa mbalimbali, kutengeneza dawa, chanjo pamoja na kutumia mafunzo ya Bioteknolojia katika kuongeza uzalishaji kwenye Viwanda lakini pia ufanyaji wa tafiti mbalimbali", alisema Prof. Kasanga

Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo kinatoa wataalamu ambao ni wahitimu wa kozi hii ya Bioteknolojia. Wahitimu hawa wakipatiwa ajira wanaweza kufanya vizuri katika maeneo ambayo yanaweza kuisaidia nchi hasa uchumi wa viwanda na Afya za binadamu na hivyo kuleta tija kubwa ndani ya Taifa .letu.



# Washauri na Walezi wa Wanafunzi SUA Watakiwa kutambua wajibu wao



*Naibu Makamu Mkuu wa Chuo (Mipango, Utawala na Fedha) Prof. Amandus Muhairwa akiongea wakati wa Semina ya siku moja ya Washauri na Walezi wa wanafunzi katika Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo.*

Washauri na Walezi wa wanafunzi katika Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo wametakiwa kutambua wajibu wao kama washauri, walezi na waelekezaji kwa wanafunzi ambao ndio wateja wakubwa chuoni hapo ili kutoa huduma stahiki kwa wanafunzi pamoja na kutatua changamoto zinazowakabili.

Wito huo ulitolewa na Naibu Makamu Mkuu wa Chuo (Mipango, Utawala na Fedha) Prof. Amandus Muhairwa, siku ya Ijumaa tarehe 19 Agosti, 2022 wakati akifungua Semina ya siku moja ya Washauri na Walezi wa wanafunzi katika Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo.

Alisema wakiwa kama Walezi na Washauri kwa wanafunzi wao ni wasaidizi wa karibu sana na Menejimenti ambapo kazi yao kubwa ni kufikisha maamuzi ya muhimu ya Chuo kwa wanafunzi, wafanyakazi, watoa huduma, wafadhili pamoja na jamii kwa ujumla hivyo wanatakiwa kutambua kuwa wao ni watu muhimu na wakutegemewa.

Prof. Muhairwa alisema kuwa ustawi wa wanafunzi ni ujumla wa shughuli zote zinazohusu maendeleo ya wanafunzi chuoni ikiwemo maendeleo ya kitaaluma, maono yao pamoja na maendeleo ya kihisia (Emotional Development) hivyo wanatakiwa kutambua kuwa wanafunzi wengi wanaenda chuoni wakiwa katika kipindi muhimu cha ukuaji na baadhi yao wapo kwenye hatua ya malezi na wakiwa ni kundi la muhimu sana ndani ya Chuo hivyo wanatakiwa kuangaliwa kwa ukaribu zaidi.

"Tunatarajia mtu wa miaka 19 hadi 25 anakuwa anamalizikia katika kulelewa au kutengenezwa ndio maana Emotional Development kubwa huwa inatokea katika kipindi hicho na ukweli usiopingika ni kwamba Dunia inaenda kasi sana hivyo kijana wa miaka ya 90 si sawasawa na kijana wa miaka ya 2020 na inaonesha wazi kabisa mbinu za kutatua changamoto zinatofautiana hivyo watumie Semina hiyo kukumbushana mbinu sahihi za kutatua changamoto hizo" alisema Prof. Amandus Muhairwa.

Aidha Prof. Muhairwa alisema wanahitaji wanafunzi zaidi kuliko wanafunzi wanavyowahitaji wao hivyo hawana budi kuwatunza na kuwatumikia vizuri wateja wao na watambue kuwa dira na maono ya Chuo vinalenga kwenye ustawi wa wanafunzi kwa sehemu kubwa.

Aliongeza kuwa sifa adhimu za washauri na walezi wa wanafunzi chuoni ili kuhakikisha azma na mipango ya Chuo inatimia kwa kuwa wasikivu wazuri ambao wanajali na kujiheshimu, wastahimilivu kwa maana ya kufanya kazi mazingira yoyote yale, wabunifu na wenye maamuzi ya haraka yenye tija, kuingilika kwa urahisi ili kutoa nafasi ya kuwawezesha wanafunzi kujieleza, waadilifu, nadhifu pamoja na wasiri.



*Mlezi wa wanafunzi SUA Bi. Hilda John akiongea neno wakati wa Semina ya siku moja ya Washauri na Walezi wa wanafunzi katika Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo.*

# Prof. Mwatawala amekipongeza Chama cha Wanataaluma SUA (SUASA)



*Naibu Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo upande wa Taaluma, Utafiti na Ushauri wa Kitaalamu Prof. Maulid Mwatawala akiongea wakati akifungua mafunzo ya kuwajengea uwezo Wanataaluma SUA ya namna ya kuandika Maandiko ya miradi ya tafiti lakini pia kupata ujuzi wa kuandika machapisho ya kisayansi.*

Menejimenti ya Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA) imepongeza jitihada zinazochukuliwa na Chama cha Wanataaluma SUA (SUASA) kwa kuwajengea uwezo Wanataaluma wake wachanga kupata mbinu na ujuzi wa kuandika maandiko yatayowasaidia kupata fedha za kufanya tafiti mbalimbali ambazo zinachangia katika kuwakuza kitaaluma.

Pongezi hizo zilitolewa na Naibu Makamu Mkuu wa Chuo upande wa Taaluma, Utafiti na Ushauri wa Kitaalamu Prof. Maulid Mwatawala wakati akifungua mafunzo ya kuwajengea uwezo Wanataaluma wa SUA ya namna ya kuandika Maandiko ya miradi ya tafiti lakini pia kupata ujuzi wa kuandika machapisho ya kisayansi.

Prof. Mwatawala aliwapongeza wawezeshaji wa mafunzo hayo ambao wengi ni wabobezi kwenye maeneo mbalimbali ya kitaaluma kwa kuamua na kukubali kutenga muda wao na kutoa, uzoefu, ujuzi na mbinu mbalimbali walizonazo kwa kizazi kipya cha Wanataaluma wa SUA.

Kwa upande wake, Mkurugenzi wa Shahada za Juu, Utafiti, Uhawilishaji wa Teknolojia na Ushauri wa Kitaalamu Prof. Esron Kalimuribo aliwataka wote walioshiriki tukio hilo kuzingatia mafunzo waliyopatiwa.

Alishukuru uongozi wa SUASA kwa kufanikisha mafunzo hayo muhimu ambayo yanakwenda kuwapa ujuzi na maarifa yatakayowasaidia katika kutafuta fedha za tafiti watakazozifanya kupitia maandiko mbalimbali duniani.

Kwa upande wake, Katibu Mkuu wa SUASA Sixbert Mourice alieleza kuwa Chuo kina mkakati wa kuwawezesha watu wake kufanya tafiti kupitia mapato ya ndani ambapo imegundulika kwamba watu wengi wanakosa miradi hiyo kutokana na ushindani mkubwa wa maandiko yanayoandikwa.

"Tumeandaa mafunzo ya siku mbili ambayo lengo lake kuwajengea uwezo Wanataaluma hasa wale wanaoingia katika utumishi wa kitaaluma ili wapate uwezo waweze kushindania miradi kutoka kwa wafadhili mbalimbali ndani ya Chuo, nchini na nje ya nchi na tunatarajia kufanya hivyo tena kwasababu kwenye mpango mkakati wetu tumepanga kuwa tutakuwa tukifanya mara mbili katika kila mwaka wa kitaaluma", alisema Sixbert.

# Umoja wa Wakulima Msoga watembelea SUA kujifunza Kilimo cha kisasa



*Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo Prof. Raphael Chibunda (kushoto) akiongea na Wakulima kutoka Msoga mkoani Pwani waliokuja SUA kwa ajili ya kujifunza Kilimo cha kisasa.*

Siku ya Jumamosi, Tarehe 10 Septemba 2022, Umoja wa Wakulima wa Umwagiliaji Msoga (UWAWAUM) kutoka Halmashauri ya Chalinze Mkoani Pwani walitembelea Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA) kwa lengo la kujifunza na kujionea kwa macho shughuli mbalimbali za kilimo hususani kilimo cha mboga.

Wakulima hao wakiwa wameambatana na viongozi wao walipokelewa na Makamu Mkuu wa Chuo, Profesa Raphael Chibunda ambaye pamoja na mambo mengine aliwasihi waendelee kushirikiana na SUA katika shughuli zao za kilimo pindi watakapo wahitaji lengo likiwa ni kuinua Kilimo nchini na kukifanya kuwa endelevu.

Profesa Chibunda alisema ni vyema kukifanya kilimo kuwa cha kisasa kwa kujifunza mbinu mbalimbali za kilimo hasa katika matumizi ya Miundombinu ya umwagiliaji na kuondokana na dhana ya kutegemea mvua pekee kwa ajili ya kilimo.

Kwa upande wake, Mwenyekiti wa UWAWAUM Bw. Joel Yohana Kipandwa amesema ziara yao ndani ya SUA ni yamafanikio makubwa kwani imewawezesha kujionea na kujifunza mambo mbalimbali katika kilimo hivyo kupitia ziara hiyo wataenda kuwa chachu na kuhakikisha wanatumia mafunzo waliyopata kuboresha Miradi yao ya kilimo waliyonayo .

Bw. Gerald Francis Muyuwa, ambaye ni Makamu Mwenyekiti wa UWAWAUM yeye alisema uwepo wa Taasisi kama SUA nchini ni fursa kubwa kwa wakulima kama wao, hivyo kupitia kile walichokiona na kujifunza chuoni hapa wameahidi kuwa mstari wa mbele katika kuwahamasisha wakulima kutembelea SUA ili kujifunza hivyo kupitia mafunzo watakayoyapata yatawasaidia kukifanya kilimo chao cha Asili walichokizoea kuwa cha kisasa na chenye Tija.

Naye Bi. Rehema Hamisi Mtendaji wa Kijiji cha Msoga alisema kuwa Elimu haina mwisho hata mkulima anatakiwa ajifunze kila siku lengo likiwa ni kujikwamua kiuchumi na matamanio yao ni kuona wakulima wa Msoga wanalima kilimo chenye Tija na cha Kisasa kwaajili ya maendeleo hivyo SUA imekuwa sehemu sahihi ya wao kuja kujifunza na wamejionea kwa macho mambo mazuri na ya faida kwao kama wakulima.



**"Ardhi ni Hazina"**

# SUA yanufaika na Mradi wa HEET



*Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknoloji Mhe. Adolf Mkenda akizungumza wakati wa uzinduzi wa Mradi wa Elimu ya juu kwa mabadiliko ya Kiuchumi (HEET Project ) uliofanyika jijini Dar es Salaam.*

Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo kimekuwa ni miongoni mwa vyuo Vikuu 14 vya Elimu ya juu nchini ambavyo vimenufaika na Mradi wa Elimu ya Juu kwa Mabadiliko ya Kiuchumi (HEET) ambao umezinduliwa Tarehe 13 Septemba, 2022 katika ukumbi wa Golden jubilee jijini Dar es Salaam.

Waziri wa Elimu,Sayansi na Teknolojia Prof. Adolf Mkenda ambaye ndiye alikuwa Mgeni rasmi katika uzinduzi huo alisema kuwa serikali itahakikisha inawasomesha Wahadhiri wa Vyuo Vikuu nje ya nchi kikiwemo Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo ili kusaidia kutoa Elimu yenye ujuzi na ubora ili kukabiliana na soko la ajira kimataifa.

"Mradi huu ni mkubwa na wa pekee kabisa kwani unatoa hamasa kuisukuma Tanzania katika suala zima la Elimu pamoja na uboreshaji wa miundombinu ya vyuo ikiwa ni pamoja na mitaala ya kufundishia na kujifunzia" alisema Waziri Mkenda.

Mhe. Mkenda pia aliwataka Viongozi wa Vyuo Vikuu vilivyonufaika na Mradi huo kutumia fedha za mradi huo kama ilivyokusudiwa ikiwemo kuboresha miundombinu ya Elimu ambayo ndio chachu ya kutoa Elimu iliyo bora kwa Wanafunzi.

Kwa upande wake Katibu Mkuu wa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia Dkt. Francis Michael aliwasisitiza wasimamizi wa mradi huo kuhakikisha wanasimamia vyema na kuhakikisha fedha za mradi zinatumika kulingana na malengo yaliyokusudiwa na ikibainika kuna ujanja watakaohusika watachukuliwa hatua za kisheria.

Naye Dkt. Winfred Mbungu ambaye ni msimamizi wa Mradi wa HEET kutoka katika Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo alisema , Chuo kitanufaika katika maeneo saba ambayo ni pamoja na ujenzi wa majengo na ukarabati wa majengo ya zamani, udhamini wa masomo kwa wafanyakazi kwa kozi za muda mrefu na muda mfupi, kuongeza uwezo wa SUA katika kuongeza mapato ya ndani vilevile mradi utasaidia watu wenye mahitaji maalum.

Jumla ya Dola za Kimarekani Milioni 425 zimetolewa kwa ufadhili wa Benki Kuu ya dunia kuhakisha mradi huo unatekelezwa chini ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia.




"Ardhi ni Hazina"

# SUA yaiomba (PSSSF) kutangaza Kilimo kwa wafanyakazi ili wanufaike na Fursa za Kilimo



*Naibu Makamu Mkuu wa Chuo Taaluma, Utafiti na Ushauri wa Kitaalamu Prof. Maulid Mwatawala, akiongea wakati wa Semina muhimu kwa wafanyakazi wa SUA kuhusiana na uelewa juu ya mabadiliko ya Kikotoo kwa wastaafu.*

Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo SUA kimeuomba Mfuko wa Pensheni kwa Watumishi wa Umma, (PSSSF) kutangaza huduma za kilimo zinazotolewa na Chuo hicho kwa wafanyakazi pindi wanapotoa elimu kuhusu Mafao ya kustaafu ili wafanyakazi hao waweze kunufaika na fursa mbalimbali za kilimo ikiwemo mafunzo yanayotolewa na SUA.

Ombi hilo lilitolewa na Naibu Makamu Mkuu wa Chuo Taaluma, Utafiti na Ushauri wa Kitaalamu Prof. Maulid Mwatawala, akimuwakilisha Makamu Mkuu wa Chuo wakati akifungua Semina muhimu kwa wafanyakazi wa SUA kuhusiana na uelewa juu ya mabadiliko ya Kikotoo kwa wastaafu iliyofanyika siku ya Ijumaa Tarehe 13 Septemba, 2022 katika Ukumbi ya Multipurpose Kampasi ya Edward Moringe (Kampasi Kuu) Morogoro.

"Chuo chetu ni Chuo Kikuu cha Kilimo na kina fani nyingine kwa hiyo sio mbaya kule mnapoenda kutoa elimu kwa hao wanaokaribia kustaafu mkawaambie kuwa wakikipata hicho kikokotoo basi wawekeze katika fursa mbalimbali za Kilimo kama vile kilimo cha bustani, utengenezaji wa Samani na kadhalika", alisema Prof. Mwatawala.

Kwa upande wake Meneja wa Matekelezo kutoka PSSSF anayeshughulikia uandikishwaji wa wanachama pamoja na Michango Bw. Victor Kikoti alisema faida kubwa zaidi kuhusiana na Kikokotoo kipya kwa wastaafu ni kuwa na mfuko endelevu ambapo kupitia kikokotoo hicho mfuko utaweza kulipa wastaafu wa sasa, wastaafu wa kesho ambao kwasasa bado ni vijana na wanaoajiriwa.

Amesema kupitia kikokotoo kutakuwa na Pensheni ambayo itatazama moja kwa moja hali ya Uchumi na kuwapandishia pensheni kila baada ya miaka mitatu wastaafu wote waliojiandikisha ambapo pia mfuko utatoa dhamana ya pensheni kwa wategemezi wake kisheria pindi mstaafu anapofariki.

"Pensheni hii inayoenda kulipwa na Kikokotoo imetathminiwa kuzingatia michango aliyochanga mstaafu, kipindi alichochanga na hali ya maisha ya nchi yetu na kama nilivyoeleza kwenye semina walikuwepo Vyama vya Wafanyakazi na Wawakilishi wa Waajiri ambao katika tathimini yao wameangalia hali ya uchumi, hali ya maisha na uendelevu wa mfuko hivyo niwatoe hofu kwani Wataalam kwa kushirikiana TUCTA wametazama hali ya maisha na wakazingatia kwamba tutaweza kuishi na mfuko utaweza kutulipa leo, kesho na hata baadae", alisema Victor Kikoti.

Naye Prof. Yasinta Muzanila alisema kuwa yeye kama mstaafu mtarajiwa na mshiriki katika semina hiyo amepata uelewa wa kutosha juu ya Kikokotoo kwani kuambiwa kitu na mhusika kimempatia taarifa sahihi na za uhakika na kumtoa wasiwasi.

Semina hiyo ya siku moja iliandaliwa na Chama cha Wafanyakazi RAAWU Tawi la SUA kwa lengo la kuwawezesha Wafanyakazi wa Chuo hicho kupata elimu juu ya mabadiliko ya kikokotoo kinachotumika kwa wastaafu.



**"Ardhi ni Hazina"**

# Mradi wa AGROVEG waendesha mafunzo kwa wakulima juu ya matumizi ya mbinu za Kilimo Ikolojia



*Kiongozi wa mradi wa AGROVEG, ambaye pia ni Mhadhiri kutoka SUA, Dkt. Ramadhani Majubwa akiongea na Wakulima (hawaonekani pichani) kuhusu umuhimu wa Kilimo Ikolojia.*

Mradi wa AGROVEG (ambao kirefu chake ni Agroecological Methodology in Vegetable crops), uliopo chini ya Idara ya Mimea Vipando na Kilimo cha Bustani wa Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo umeendesha mafunzo ya siku 3 kuanzia tarehe 11 hadi 13 Septemba, 2022, kwa wakulima kutoka kata za Mlimani, Kinyenze, Vitonga, Mlali na Kiroka mkoani Morogoro kwa lengo la kuwapatia mbinu mbalimbali za kilimo ikolojia.

Wakulima hao walifundishwa na kuonyeshwa matumizi ya Kilimo Ikolojia katika uzalishaji wa mazao mbalimbali ya Mboga, mbinu ambazo zitawasaidia wakulima hao kupunguza matumizi ya pembejeo za viwandani kwa kiasi kikubwa, hivyo kulinda Afya ya Mlaji na Mkulima.

Akizungumza wakati wa Mafunzo hayo, Kiongozi wa mradi huo wa AGROVEG, ambaye pia ni Mhadhiri kutoka SUA, Dkt. Ramadhani Majubwa alieleza kuwa Kilimo Ikolojia kinalenga hasa kuhakikisha mkulima anatumia mbinu rafiki ambazo zinatunza mazingira pamoja na kutunza viumbe hai ambao wanapatikana katika eneo husika.

"Tumelenga kufundisha wakulima kuzalisha mazao ambayo hayatakuwa na sumu na kuwapunguzia athari zinazoweza kutokea kutokana na upuliziaji wa dawa shambani ambazo mara nyingi dawa hizo huweza kuwarudia wenyewe na kuweza kusababisha athari za kiafya", alisema Dkt. Majubwa.

Aliwataka wakulima kuacha kulima kwa mazoea na badala yake kuanza kutumia mbinu za Kilimo cha Ikolojia kwa sababu njia hiyo itawasaidia kukabiliana na mabadiliko ya tabia nchi yanayo endelea kutokea duniani, Kupunguza gharama zinazotumika kwenye manunuzi ya pembejeo, na kuongezeka kwa uzalisahaji wa mazao kutokana na kuongezeka kwa wadudu rafiki kama vile nyuki ambao husaidia katika uchavushaji.



**"Ardhi ni Hazina"**

# SUA kupitia Maktaba ya Taifa ya Sokoine ya Kilimo kuanzisha Kitabu kiitwacho “Kilimo cha Kisasa Mkononi Mwako (Mboga App)”




*Jengo la Maktaba ya Taifa ya Sokoine ya Kilimo lililopo Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo.*

Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo kupitia Maktaba ya Taifa ya Kilimo iliyopo chuoni hapo imeanzisha kitabu chenye jina la Kilimo cha Kisasa Mkononi Mwako (Mboga App), chenye lengo la kuwafundisha vijana mbinu mbalimbali za uzalishaji wa mbogamboga ili kujiajiri kupitia Sekta ya Kilimo.


Akizungumza kupitia kipindi cha Kapu la Leo Septemba 20, 2022 Afisa Maktaba Bw. Shabani Omary Chika alisema kitabu hicho ni moja kati ya hazina walizoaamua kuonesha kwa vijana ambazo zinaweza kuwa muarobaini wa vyanzo vidogovidogo vya mapato na ndani ya hazina hiyo kuna maarifa yaliyojificha yanayoweza yakamfumbua macho kijana na kumtoa kutoka hatua moja kwenda nyingine.

Aidha, Bw. Chika alisema kuwa vijana wamekuwa wakilalamika kuhusu ugumu wa maisha lakini kupitia kitabu hicho anaweza kujifunza jinsi ya kuotesha mbogamboga akiwa nyumbani hata kama ni katika eneo finyu.


“Hichi kitabu pamoja na kuwa kipo kwa nakala ngumu lakini pia kuna “application” ambayo vijana wengi wamekuwa na simu janja hivyo anaweza kuingia katika simu janja yake akaenda kwenye "play store" akaandika Mboga App akaipakuwa na ikampa mazingira yote juu ya namna ambavyo anaweza kulima, namna ambavyo anaweza akaandaa kitalu namna ya kuotesha kitalu na vitu vyote vimeelezwa katika app hii”. Alieleza Bw. Chika.

Kwa upande wake Bi. Editha Njeu ambaye pia ni Afisa wa Maktaba ya Taifa ya Sokoine ya Kilimo, alieleza kuwa kitabu hicho kimeonesha mambo mbalimbali ikiwemo kujua uchaguzi wa eneo lenye uwezo wa kumudu upatikani wa mbolea, maji pamoja na wateja ili kuepuka gharama.

Kitabu hicho kimeandikwa na Mkufunzi kutoka chuoni hapo Teophilda J. Maginga kimetoa elimu kwa wakulima na namna ya kupunguza gharama ikiwa ni pamoja na matumizi ya dawa za asili kama vile kupanda miti au majani mbalimbali yanayoweza kufukuza wadudu ili kuepuka kuingia gharama hasa kwa vijana wasio na mtaji.



# SUA kukabiliana na Changamoto za Uhaba wa Malisho, Uharibifu wa Mazingira na Ukosefu wa Ajira Tanzania.




Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo kupitia wataalam wake wameendelea kufanya juhudi za kutatua changamoto za uhaba wa malisho, uharibifu wa mazingira na ukosefu wa ajira kwa wanawake na vijana na wameanza utekelezaji wa mradi wa Tekinolojia ya Juncao kwa kuanza kuzalisha na kusambaza mbegu za nyasi aina Juncao Tanzania Bara na visiwani Zanzibar.

Teknolojia hii inahusisha matumizi ya nyasi aina ya JUNCAO katika uzalishaji wa uyoga, kuhifadhi ardhi, kuzuia mmomonyoko wa udongo, pamoja na malisho kwa ajili ya mifugo ambapo asili yake ni kutoka Chuo Kikuu cha Kilimo na Misitu (FAFU) kilichoko Jimboni Fujian, nchini China.

Akizungumza na SUAMEDIA siku ya Jumanne tarehe 20 Septemba 2022, Mtaalamu wa teknolojia ya JUNCAO kutoka Idara ya Sayansi za Elimu ya Viumbehai (Biosciences), Ndaki ya Sayansi Asilia na Tumizi ya SUA, Dkt. Elly Ligate alisema kwamba kushirikiana na watafiti na maafisa kilimo visiwani Zanzibar wameanzisha vitalu vya nyasi hizo katika mashamba ya majaribio yaliyoko katika kituo cha utafiti wa mifugo kilichopo Kizimbani Unguja na Chamanangwe kisiwani Pemba.

“Juhudi za kutekeleza Teknolojia ya Juncao nchini zilianza mwanzoni mwa mwaka 2021 na zimeendelea kuenea nchi nzima na Kila tuliko peleka mbegu wakulima wameonesha kuzikubali” alisema Dkt. Ligate

Aliendelea kwa kusema kuwa kwa upande wa Tanzania bara wataalamu kutoka SUA wameshirikiana na Wizara ya Mifugo na Uvuvi kufanya majaribio ya uzalishaji wa nyasi hizo katika wilaya zipatazo 11 kwenye mikoa tofauti, Mbegu za Nyasi za Juncao zimeshasambazwa kwa wakulima katika wilaya za Geita, Kilindi, Handeni, Kibaha, Kigamboni, Bumbuli, Chalinze, Kilosa, Bahi, Mbarali, Dodoma pamoja na Ubungo na Kinondoni.

Dkt. Ligate alifafanua kwamba vituo hivi vitatumika katika kuzalisha mbegu za kutosha ili ziweze kusambazwa kwa wakulima na wafugaji nchini Tanzania ambapo Matarajio yao makubwa ni kuwafikia wafugaji wengi katika visiwa vya Zanzibar na Tanzania Bara kwa kuwa mahitaji ya malisho ni makubwa katika kuelekea kuimarisha sekta ya mifugo nchini.

Dkt. Ligate alitoa shukrani kwa Wizara ya Mifugo na Uvuvi Tanzania bara, Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo ya Zanzibar, Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA), Chuo Kikuu cha Fujiani cha Kilimo na Misitu (FAFU), pamoja na wadau binafsi kama vile Ndugu Albert Marwa kwa kufanikisha kuenea kwa tekinolojia ya Juncao nchini Tanzania.

# Balozi wa Uganda apongeza utafiti wa majani ya JUNCAO



*Balozi wa Uganda nchini Tanzania Kanali Fred Mwesigye (kulia) akizungumza na baadhi ya Watumishi wa Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo wakati wa ziara yake ya siku moja katika Kampasi ya Solomon Mahlangu.*

Balozi wa Uganda nchini Tanzania Kanali Fred Mwesigye, amepongeza utafiti wa majani ya JUNCAO ambayo ni teknolojia kutoka nchini China iliyoletwa nchini Tanzania na watafiti wa Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo.

Pongezi hizo alizitoa septemba 23, 2022 katika kampasi ya Solomoni mahlangu, kwenye ziara yake ya siku moja Chuoni hapo ambayo imelenga kufahamu kwa kina Teknolojia hiyo kutoka SUA, akiongozwa na Mhadhiri mwandamizi na mtaalamu wa teknolojia ya JUNCAO kutoka Idara ya Sayansi za Viumbe hai, Ndaki ya Sayansi Asilia na Tumizi ya SUA, Dkt. Elly Ligate pamoja na Mhadhiri mwandamizi katika Idara hiyo ambaye pia ni Mkuu wa Idara Dkt. Beda Mwang'onde.

“Nawashukuru sana viongozi wa Chuo hiki kuniita kuja kuwatembelea kuona nyasi za JUNCAO. mimi kwa upande wangu nafikiri tutafaulu sana kwa kuwa huko Uganda tunafuga sana ng'ombe zamani tulikuwa kama masai lakini kwa sasa tunafanya ufugaji wa kisasa hivyo tutashirikiana na ninyi kuhakikisha tunaitambulisha teknolojia hii Uganda” Alisema balozi Mwesigye.

Kwa upande wake mtaalamu wa teknolojia ya JUNCAO kutoka SUA, Dkt. Elly Ligate, alisema kwa sasa wamefika Uganda lakini matamanio yao ni kufika nchi nyingine za jirani ambapo teknolojia hii itahitajika, lakini nchini Tanzania hadi hivi sasa wamefanikiwa kuwafikia wakulima wapatao 54 katika wilaya zaidi ya 10 ambazo ni Kilindi, Handeni, Bumbuli, Geita, Bukoba, Kagera, Mbarali, Dodoma, Kigamboni, Pwani, Morogoro na hata Kilosa.


“Ziara hii tunaichukulia kwa umakini wa hali ya juu sana kwasababu ni ziara ambayo inaongeza wigo wa matokeo ya teknolojia hii ambayo inaenda kuleta majibu katika sekta ya ufugaji kutokana na kuwa na changamoto ya malisho haipo tu Tanzania bali Afrika ya Mashariki kwa ujumla na kwa sababu tuna mahusiano ya kimataifa na Taasisi zingine kama vile Chuo Kikuu cha Kilimo na Mifugo kilichopo nchini China tunaamini teknolojia hii itafika mbali zaidi”. Alisema Dkt. Ligate

Aidha, ametoa wito kwa wakulima kuwa kulima nyasi za JUNCAO ni fursa kwa ajili ya kuwauzia wafugaji hasa zama hizi ambazo kuna mabadiliko ya tabia ya nchi na ongezeko la matumizi ya ardhi, kutokana na nyasi hizo kuwa na ustahimili wa kulimwa kwenye maeneo ya jangwa na hata majira ya kiangazi.

Kwa upande wake Mhadhiri Mwandamizi kutoka Idara ya Sayansi za Viumbe hai na Mkuu wa Idara hiyo Dkt. Beda Mwang'onde amesema kutokana na kuwa wanyama tulionao ni wengi na malisho haba nyasi za JUNCAO zitaweza kutokomeza ufugaji wa kuhamahama ambao unapelekea familia nyingi za wafugaji kutelekezwa na hata watoto kutopata elimu.

Akizungumza baada ya kumaliza ziara hiyo, Balozi Mwesigye amesema nchi yake itaendelea kushirikiana na Tanzania kwenye maeneo mbalimbali na kupitia SUA wataona namna ya kuitambulisha na kuisambaza zaidi teknolojia hii ya nyasi za JUNCAO nchini Uganda kwa lengo la kutatua migigiri ya wakulima na wafugaji nchini humo.

# Prof. Sibuga: "Mkutano wa "CROSAT" utasaidia kuunganisha Wadau wa Kilimo"




*Mwenyekiti wa Umoja wa Wanasayansi wa Mazao na Vipando Tanzania (CROSAT) Prof. Kalunde Sibuga (katikati, waliokaa) akiwa kwenye picha ya pamoja na wadau wengine waliohudhuria mkutano wa umoja huo uliofanyika mkoani Dodoma akiwemo Naibu Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo upande wa Taaluma, Utafiti na Ushauri wa Kitaalam Prof. Maulid Mwatawala (wa kwanza kushoto, waliosimama).*

Imeelezwa kuwa Mkutano wa Mwaka wa Umoja wa Wanasayansi wa Mazao na Vipando Tanzania (CROSAT] utasaidia kwa kiasi kikubwa kuunganisha Wataalam wa Kilimo, Wakulima na Makampuni yanayo husika na uchakataji wa mazao ya Kilimo na kuishauri Serikali kuhusu masuala mbalimbali yanayohusu Mazao.

Hayo yalielezwa na Mwenyekiti wa CROSAT Prof. Kalunde Sibuga ambaye pia ni Mhadhiri wa Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA) wakati akizungumza na SUAMEDIA siku ya Alhamisi tarehe 22 Septemba, 2022 jijini Dodoma kuhusu umuhimu wa Mkutano huo katika Ustawi wa Kilimo nchini.

Prof. Sibuga pia alisema kuwa CROSAT inapanga mikakati ya pamoja kuhusu kuboresha Katiba yao ili kuongeza tija katika kilimo cha mazao.

Aidha Prof. Sibuga amesema CROSAT inaunganisha Wataalam wa Kilimo, Wakulima, Makampuni yanayo husika na Uchakataji wa mazao ya Kilimo pamoja na Taasisi zinazo husika na masuala mbalimbali yanayohusu kilimo.

Kwa upande wao baadhi ya Washiriki wa Mkutano huo Patroba Bwire Masatu ambaye ni Mwanafunzi wa Shahada ya Uzamivu (PhD) SUA na Jenipher Tairo anayesoma Shahada ya Uzamili katika Sayansi ya Kilimo na Mimea walisema CROSAT ni Jukwaa ambalo linawaunganisha Wanasayansi wa Mazao na Vipando Tanzania na wadau wote kuweza kuwa na Lugha moja katika ustawi wa Kilimo.

Aidha Washiriki hao pia waliomba wale ambao bado hawajajiunga na CROSAT waweze kujiunga na umoja huo ili kupata jukwaa imara kwa maslahi mapana ya Taifa na Jumuiya ya Kimataifa kwa ujumla maana Kilimo ndio Sekta pekee inayo ajiri watu wengi nchini.



# SUA, RECODA na ADRA zaja na Mradi wa Kilimo na Masoko



*Rasi wa Ndaki ya Sayansi za Jamii na Insia, Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo Prof. Kabote aliyekaa katikati akiwa katika picha ya pamoja na wadau wa utafiti wa mradi wa Kilimo na Masoko, kulia ni Mkurugenzi wa ADRA-Tz Bw. Samwel Oyortey na kushoto waliokaa ni Dr. Dominick Ringo Mkurugenzi wa RECODA.*

Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA) kwa kushirikiana na Mashirika yasiyo ya Kiserikali ya RECODA, ADRA Tanzania na ADRA Denmark, zimetekeleza mradi wa majaribio wa kuwajengea wakulima uwezo wa uzalishaji wenye tija na namna bora ya kuuza mazao yao. SUA kwa upande wake ilijikita zaidi katika kipengele cha utafiti ambao umeonesha kuwepo matokeo chanya na kuwa mifumo ya RIPAT na FMS kwa pamoja inamsaidia mkulima kuzalisha mazao bora na kuwa na uhakika wa masoko.

Akizungumza Septemba 23, 2022 katika warsha ya siku moja ya kuwasilisha matokeo ya utafiti wa Mradi wa Kilimo na Masoko, Rasi wa Ndaki ya Sayansi za Jamii na Insia, Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA) Prof. Samwel Kabote alisema endapo mfumo huu utaendelea kufanya kazi kwa ufanisi basi utaleta mapinduzi makubwa katika kilimo na masoko nchini

“Kwa upande wa utafiti mradi unatafiti juu ya uunganishwaji wa RIPAT (Rural Initiatives for Participatory Agricultural Transformation), yaani Jitihada Shirikishi za Kuleta Mageuzi ya Kilimo Vijijini, na FMS (Farmer Market School), yaani Shule ya Soko la Mkulima na matokeo yake kwenye kipato na uhakika wa chakula kwa wakulima wadogo” alisema Prof. Kabote

Alisema mifumo hii miwili ya RIPAT na FMS iliyotumika kwenye mradi wa Kilimo Masoko itawajengea wakulima uwezo wa kuzalisha na kuuza mazao yao na matokeo yake ni kuongeza kipato na uhakika wa chakula kwa wakulima wadogo.

Akitoa mrejesho wa utafiti huu, Mratibu wa mradi huo kwa upande wa SUA, Dkt. Emmanuel Malisa alisema ili kuhakikisha kunakuwa na uzalishaji wenye tija na upatikanaji wa masoko kunahitajika juhudi zaidi ya sasa ili kwenda mbali zaidi ya mashamba ya maonyesho na mafunzo katika ngazi za vikundi pekee.

Dkt. Malisa alisema utafiti umeonyesha kuwa, kupitia mifumo hii miwili ya RIPAT na FMS, kuna uwezekano mkubwa wa mkulima mdogo kuboresha maisha yake, kuongeza kipato na kuwa na uhakika wa chakula.

Amesema wakulima waliokua katika vikundi vya kuweka na kukopa (VSLA) walikuwa na uwezekano mkubwa wa kuwa na mseto mkubwa wa chakula zaidi ikilinganishwa na wasio wanachama.

“Wakulima waliotumia vyakula bora vya kulishia mifugo yao (mbuzi wa maziwa, kuku na nguruwe) walikuwa na nafasi ya 75% ya kupata chakula cha aina nyingi zaidi kuliko wenzao. Wakulima hawa waliongeza uwezekanno wa kupata nyama, mayai, na maziwa” alisema Dkt. Malisa.

Aidha alisema matumizi ya chanjo ya kuku, mbegu bora, umwagiliaji ili kukabiliana na ukame na kuwa na mizunguko mingi ya uvunaji, na uuzaji wa mazao kwa pamoja kunaweza kumuinua mkulima kwa kiasi kikubwa.

Naye Mkurugenzi wa RECODA (Research, Community and Organizational Development Associates), Dkt. Dominick E. Ringo alisema mfumo wa RIPAT unatumika maeneo mengi nchini Tanzania, pamoja na nchi nyingine kama Kenya, Burundi, Rwanda na Nicaragua, na umeonesha mafanikio katika kuziba pengo la teknolojia za kilimo.

Kwa upande ADRA Tanzania, Mkurugenzi wa shirika hilo, Bw. Samuel Oyortey alisema mfumo wa FMS umefanya vizuri Malawi, Zimbabwe na Uganda, na sasa kupitia mradi wa Kilimo na Masoko unafanyiwa majaribio Tanzania.

# Wafanyakazi SUA watakiwa kushiriki kwa wingi Chibunda CUP



*Rasi wa Ndaki ya Sayansi ya Jamii na Insia Prof. Samwel Kabote akisalimiana na wachezaji wa mpira wa miguu wakati wa ufunguzi wa michuano wa watumishi wa  Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo maarufu kama Chibunda Cup.*







Wafanyakazi wa Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo wametakiwa kujitokeza kwa wingi katika kushiriki michuano ya michezo mbalimbali ya watumishi, maarufu kama Chibunda Cup.

Wito huo ulitolewa na Rasi wa Ndaki ya Sayansi ya Jamii na Insia Prof. Samwel Kabote akimwakilisha Makamu Mkuu wa Chuo wakati wa ufunguzi wa msimu wa 6 wa michuano hiyo siku ya Ijumaa Tarehe 23 Septemba, 2022 kwenye viwanja vya michezo vya Kampasi ya Edward Moringe (Kampasi Kuu).

“Mashindano haya ya wafanyakazi yanasaidia kuwaweka wafanyakazi pamoja lakini pia yanasaidia kuimarisha Afya za wafanyakazi wetu kwa hiyo niwaombe wafanyakazi wote tujumuike kwa pamoja kwenye mashindano haya." Alisema Prof. Kabote.

Pamoja na hayo Prof. Kabote aliongeza kuwa mashindano hayo yamekuwa yakifanyika kila mwaka na yamendelea kuwa na matokeo chanya kwa kuongeza mahusiano mazuri baina ya wafanyakazi na utendaji kazi katika chuo hicho.

Michezo iliyochezwa siku hiyo ya ufunguzi ni pamoja na Mpira wa Miguu , Mchezo wa kuvuta Kamba pamoja na Mchezo wa Mpira wa pete kwa Wanawake .








## Imetolewa na:-

IDARA YA MAWASILIANO NA MASOKO
S.L.P. 3000, CHUO KIKUU, MOROGORO, TANZANIA
Simu: 255-023-2640006/7/8/9,
Direct Line: 255-023-2640018
Barua pepe: communicationandmarketing@sua.ac.tz

**"Ardhi ni Hazina"**